# MKATABA WA UPANGISHAJI WA CHUMBA CHA BIASHARA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 22 Mwezi wa 08 Mwaka 2023

**KATI YA**

**SANGA FRESH INVESTMENT LIMITED** wa **S.L.P 1227 MBEYA** (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama **MPANGISHAJI** neno ambalo litajumuisha na warithi wake) kwa upande mmoja.

**NA**

**PRIDE OF NILE PVT LIMITED wa S.L.P**......1966......

(ambaye katika mkataba huu anajulikana kama **MPANGAJI** neno ambalo litajumuisha na warithi wake) kwa upande mwingine.

Kwa vile **MPANGISHAJI** ana nia ya kupangisha chumba cha biashara yake kwa **MPANGAJI** na kwa vile **MPANGAJI** anayo nia ya kupanga chumba hicho cha biashara kilichopo eneo la kata ya Izigo wilaya ya Muleba na Mkoa wa Kagera, basi pande zote mbili zimekubaliana kama ifuatavyo:-

1. Kwamba **(MPANGISHAJI)** kwa hiari yake ameamua kumpangisha **(MPANGAJI)** Chumba Cha Biashara kilichopo eneo la kata ya Izigo, Wilaya ya Muleba Mkoa wa Kagera kwa Muda wa **Miezi 6** kuanzia tarehe **22 mwezi wa 08 mwaka 2023** hadi tarehe **22 Mwezi 02 Mwaka 2024**
2. Kwamba **MPANGAJI** anatakiwa kulipa kodi ya shilingi za Kitanzania **600,000/=** (laki sita ) kiasi cha gharama ya upangaji kwa muda wa miezi sita tokea tarehe tajwa haya ya 1.
3. Kwamba kwa kuwa mpangaji anapangisha chumba hicho cha biashara kwa Miezi 6 tu atatakiwa kulipa kodi yote ambayo ni fedha za kitanzania shilingi **600,000/=** (laki sita ) tu na italipwa kwa awamu moja tu.
4. Kwamba muda wa upangaji ni Miezi 06 tu kuanzia tarehe ya upangishaji wa chumba hicho cha biashara ambayo ni tarehe 22 mwezi wa 08 mwaka 2023 mpaka tarehe 22 mwezi wa 02 mwaka 2024.
5. Kwamba endapo MPANGAJI ataamua kufufua mkataba basi atatakiwa kulipa kodi ya pango kabla ya Mwezi mmoja kumalizika kwa mkataba huu.

6. Kwamba MPANGAJI atatumia chumba hicho cha biashara hiyo kwa matumizi ya biashara tu na kama atataka kubadili matumizi ni sharti kabla ya kufanya hivyo akubaliane na MPANGISHAJI na si vinginevyo.
7. Kwamba MPANGAJI hatampangisha mtu mwingine au kuuza chumba hicho cha biashara kwa mtu mwingine bila ridhaa ya MPANGISHAJI.
8. Kwamba MPANGAJI haruhusiwi kufanya mabadiliko yoyote ya kiujenzi kwenye chumba hicho cha biashara alichopangishwa bila kuwa na idhini ya MPANGISHAJI na endapo atafanya marekebisho yoyote wakati wa kumaliza mkataba huu ataacha marekebisho aliyofanya kama yalivyo.
9. MPANGISHAJI haruhusiwi kumbughudhi MPANGAJI wake kwa namna yoyote kwa muda wote wa Upangishaji katika mkataba huu.
10. Kwamba MPANGISHAJI ataruhusiwa na MPANGAJI kukagua chumba cha biashara kinachopangishwa pale inapobidi na kwa muda wa mchana na kuangalia usalama wa chumba icho na vifaa au thamani zilizomo na hata ikibidi kufidia, kurekebisha au kununua vifaa vipya iwapo MPANGISHAJI atagundua kuwa kuna uharibifu wa aina yoyote kwenye nyumba au vifaa husika.
11. Kwamba, MPANGISHAJI hatoruhusiwa kuifadhi ndani ya chumba cha biashara vifaa hatarishi hasa vyenye asili ya mlipuko kwaajili ya usalama wa chumba hicho na vymba vingine vinavyozunguka chumba hicho alichopanga.
12. Kwamba MPANGAJI akitaka kuvunja mkataba huu, ni lazima atoe taarifa ya mwezi mmoja (1) kwa MPANGISHAJI vinginevyo hatopata kodi yake iliyosalia vivyo hivyo MPANGISHAJI atatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja (1) kufanya vinginevyo upande uliodhurika utalipwa gharama za usumbufu.
13. Kwamba kwa kuzingatia mkataba wa chumba hicho cha biashara haujaisha, MPANGISHAJI hatompangisha mtu mwingisne kwenye chumba hicho cha biashara au kuuza chumba cha biashara bila ya kumtaarifu MPANGISHAJI na kama itatokea basi haki na stahiki za MPANGAJI hazitaathiliwa kwa vyovyote vile.
14. Kwamba MPANGAJI atawajibika kulipia huduma ya Umeme na amaji atakavyotumia kwenye nyumba aliyopangishwa wakati wote wa upangaji huo.
15. MPANGAJI hataondolewa na yeyote katika chumba hicho cha biashara wakati wa uhai wa mkataba huu isipokuwa kwa MPANGAJI kuvunja moja ya masharti ya mkataba huu ama kwa MPANGAJI mwenyewe kuomba kuondoka kwenye chumba hicho cha biashara.

16. Baada ya mkataba huu kufikia ukomo wa miezi 06 MPANGISHAJI na MPANGAJI wanaweza kufanya mapatano ya kuendeleza mkataba huu kwa masharti haya au vinginevyo kwa kuzingatia kipengele namba 5 cha mkataba huu. Lakini kukiwa hakuna makubaliano yoyote hadi kuisha kwa mkataba huu, MPANGAJI atawajibika kukabidhi chumba hicho kwa MPANGISHAJI ikiwa katika hali nzuri.

17. Na kila mara wahusika wazingatie mkataba

    (a) Iwapo mmoja wa wahusika atakiuka makubaliano na masharti ya mkataba huu, atakayekiuka itabidi kulipa hasara zilizojitokeza.

    (b) Iwapo kutakuwa na kutoelewana na kwa yaliyomo katika mkataba huu kutoelewana huko kutatuliwe na sheria za Tanzania.

    (c) Migogoro mingine ikijitokeza wahusika wakishindwa kuitatua wao wenyewe basi mahakama itumike ili kutatua migogoro hiyo.

Kwa uthibitisho na ushahidi Zaidi wahusika wameweka saini zao kwenye mkataba huu tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonekana hapa chini.

Umetiwa saini na kutolewa hapa Mbeya na

**SANGA FRESH INVESTMENT LIMITED**

ambaye

ametambulishwa kwangu na

...JANETH KAIZAGY...

Ambaye namfahamu binafsi

**Leo tarehe 22 mwezi 08 mwaka2023**

.............................................

**MPANGISHAJI**

**MBELE YANGU:**

**JINA:** ...LADISLAUS RWEKAZA...

**SAHIHI:** .............................................

**ANWANI:** ...2865, MBEYA...

**CHEO:** ...WAKILI...

Ladislaus Rugemalira Rwekaza
Box 2865 Mbeya
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Umetiwa saini na kutolewa hapa Mbeya na

**PRIDE OF NILE PVT LIMITED**

ambaye

ametambulishwa kwangu na

...JANETH KARARY...

Ambaye namfahamu binafsi

**Leo tarehe………mwezi…….2023**

……………………………..

**MPANGAJI**

**MBELE YANGU:**

**JINA:** ...LADISLAUS RWEKAZA...

**SAHIHI:** ……………………………………

**ANWANI:** ...2865, MBEYA...

**CHEO:** ...WAKILI...

Ladislaus Rugemalira Rwekaza
Box 2865 Mbeya
Advocate, Notary Public
& Commissioner for Oaths